OFISI YA RAIS, IKULU
Kaunda Road S.L.P. 2422
ZANZIBAR -TANZANIA

Simu: 2230814/5
Fax: 2233722
press@ikuluzanzibar.go.tz
www.ikuluzanzibar.go.tz

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
AFISI YA RAIS, IKULU

03 Oktoba 2026
Ikulu, Zanzibar

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, ametangaza uteuzi na uhamisho wa mawaziri na naibu mawaziri, pamoja na mabadiliko ya miundo ya baadhi ya wizara, hatua inayokamilisha uundwaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa kuwajumuisha mawaziri kutoka Chama cha ACT-Wazalendo.

Rais Dkt. Mwinyi ameyasema hayo leo, tarehe 03 Oktoba 2026, katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika Ikulu Zanzibar, ambapo ameeleza hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa makubaliano ya maridhiano baina ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na ACT-Wazalendo.

Dkt. Mwinyi amesema teuzi hizo ni mwendelezo wa utekelezaji wa makubaliano baina ya CCM na ACT-Wazalendo kuhusu uundwaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Ameeleza kuwa hatua zilizotangulia ni uteuzi wa Mhe. Othman Masoud Othman kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na wajumbe wawili wa Baraza la Wawakilishi waliopendekezwa na ACT-Wazalendo.

Ameeleza kuwa ACT-Wazalendo iliwasilisha majina manne kwa uteuzi wa mawaziri, kwa kuzingatia nafasi nne za chama hicho katika Baraza la Mawaziri kwa mujibu wa Katiba.

Rais Dkt. Mwinyi amesema masuala ya Mipango yamehamishiwa Ofisi ya Rais, Ikulu. Kufuatia mabadiliko hayo, iliyokuwa Wizara ya Fedha na Mipango sasa itaitwa Wizara ya Fedha, ikiendelea kuongozwa na Mhe. Dkt. Juma Malik Akil.

Aidha, Rais Dkt. Mwinyi amesema sekta ya Kazi imehamishiwa iliyokuwa Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji, ambayo sasa itaitwa Wizara ya Kazi, Ajira, Vijana na Uwezeshaji. Kufuatia mabadiliko hayo, iliyokuwa Wizara ya Kazi na Uwekezaji sasa itaitwa Wizara ya Uwekezaji, ikiendelea kuongozwa na Mhe. Shariff Ali Shariff.

Rais Dkt. Mwinyi amefafanua kuwa Wizara ya Kazi, Ajira, Vijana na Uwezeshaji itakuwa na naibu mawaziri wawili, ambapo mmoja atasimamia Kazi na Ajira na mwingine atasimamia Vijana na Uwezeshaji.

Kwa upande wa mawaziri, Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum amehamishiwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, huku Mhe. Anna Athanas Paul akihamishiwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Shaaban Ali Othman ameteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu, anayeshughulikia Mipango na Usimamizi wa Utendaji Serikalini.

Mhe. Masoud Ali Mohamed, aliyekuwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, ameteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu, anayeshughulikia Uhusiano wa Jamii, huku Mhe. Mudrik Ramadhan Soraga akiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi.
Aidha, Mhe. Ali Suleiman Ameir Mrembo ameteuliwa kuwa Waziri wa Kazi, Ajira, Vijana na Uwezeshaji.

Vilevile, Mhe. Nassor Ahmed Mazrui (ACT- Wazalendo) ameteuliwa kuwa Waziri wa Afya, Mhe. Omar Said Shaaban (ACT- Wazalendo) kuwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, na Mhe. Dkt. Nasra Nassor Omar (ACT- Wazalendo) kuwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale.

Mhe. Dkt. Mohamed Ali Suleiman, (ACT- Wazalendo), ameteuliwa kuwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu.

Mawaziri wanaoendelea katika nafasi zao ni pamoja na:

1. Mhe. Haroun Ali Suleiman, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.
2. Mhe. Hamza Hassan Juma,Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi.
3. Mhe. Riziki Pembe Juma, Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo.
4. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.
5. Mhe. Rahma Kassim Ali, Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi.
6. Mhe. Lela Muhamed Mussa, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.
7. Mhe. Suleiman Masoud Makame, Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo.
8. Mhe. Idrissa Kitwana Mustafa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.
9. Mhe. Nadir Abdullatif Alwardy, Waziri wa Maji, Nishati na Madini.

Kwa upande wa naibu mawaziri, Mhe. Hassan Khamis Hafidh ameteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Afya, Mhe. Dkt. Hamad Omar Bakari amehamishiwa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, na Mhe. Mboja Ramadhan Mshenga amehamishiwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Aidha, Mhe. Dkt. Salum Sudi Hamid atakuwa Naibu Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Mhe. Bakari Hamad Bakari atakuwa Naibu Waziri wa Fedha, na Mhe. Juma Hassan Thabit Kaponda atakuwa Naibu Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale.

Mhe. Zawadi Amour Nassor na Mhe. Seif Kombo Pandu watakuwa naibu mawaziri katika Wizara ya Kazi, Ajira, Vijana na Uwezeshaji. Mhe. Zawadi atashughulikia masuala ya Vijana na Uwezeshaji, huku Mhe. Seif akishughulikia masuala ya Kazi na Ajira. Aidha, Mhe. Khadija Salum Ali amehamishiwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Naibu mawaziri wanaoendelea katika nafasi zao ni pamoja na:

1. Mhe. Ali Abdulgullam Hussein, Naibu Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo.
2. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma, Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi.
3. Mhe. Mohamed Sijamini Mohamed, Naibu Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu.
4. Mhe. Badria Atai Masoud, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

Mawaziri na Naibu Wawaziri wote walioteuliwa na waliohamishwa wizara wataapishwa siku ya Jumatatu, tarehe 05 Oktoba 2026, saa 8:00 mchana.

Raqey Mohamed
Kaimu Mkurugenzi, Mawasiliano, Ikulu